TANGAZO LA SERIKALI NA. 101 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA MKOMBWE NA MJIMWEMA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Mkombwe na Mjimwema ya Mwaka, 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji Mafinga.

*Tangazo la serikali na. 101 (linaendelea)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MKM 01 yenye majira - nukta 752217MS, 9082632KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.09 hadi unapokutana na barabara ya TANZAM kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MKM 02 yenye majira - nukta 754360MS, 9084780KZ; baada ya hapo mpaka unafuata barabara ya TANZAM kwa umbali wa kilomita 0.45 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MKM 03 yenye majira - nukta 754485MS, 9085216KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa kufuata barabara ya TANZAM hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MKM 04 yenye - majira nukta 754526MS, 9085343KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.39 hadi unakutana na barabara ya zamani ya Dar es Salaam kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MKM 05 yenye majira - nukta 754210MS, 9085571KZ; baada ya hapo mpaka unafuata barabara ya zamani ya Dar es Salaam kwa umbali wa kilomita 0.49 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MKM 06 yenye majira - nukta 754165MS, 9085084KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MKM 07 yenye majira - nukta 754198MS, 9085063KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.23 hadi unapokutana na barabara ya zamani ya Dar es Salaam kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MKM 08 yenye majira - nukta 754184MS, 9084835KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MKM 09 yenye majira - nukta 754207MS, 9084817KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MKM 01 hadi ulipoanzia''

Dodoma,
6th February, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*